# SHULE YA UPILI YA KITAIFA YA KAPSABET

**102/3** (***Kenya Certificate of Secondary Education***)

**3**

**MTIHANI WA MWIGO**

**KISWAHILI**

**(FASIHI)**

**Dis. 2020 – Muda: Saa 2 ½**

# MWONGOZO

**Maagizo**

a) *Andika jina lako,nambari ya usajili, mkondo katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Tia sahihi yako kisha uandike usajili na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
c) *Jibu maswali* ***manne pekee.***
d) *Swali la* ***kwanza*** *ni* ***lazima****.*
e) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki,yaani:* ***Tamthilia,Hadithi Fupi,Ushairi na Fasihi Simulizi.***
f) *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka* ***sehemu moja****.*
g) *Majibu yote sharti yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
h) *Majibu yote* ***lazima*** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
i) *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
j) ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

1. (a) (i) maneno ya Babu(Daktari) UK84
(ii) anamwambia Majoka
(iii) Majoka yuko Hospitali
(iv) Majoka alizimia baada ya kupata habari ya kifo cha mwanaye/aliwehuka akaanza kuzungumza na Daktari kana kwamba ni Babu yake- Ngao

**1X4**

(b) (i) taswira maono - binadamu anaonekana kuwa mavumbi/kukanyaga

migongo

(ii) taswira muonjo -kwa tamaa mtu anapenda kula kuku

(iii) taswira mnuso -kula kama kuku/kuku kula hata vilivyonuka

(iv) taswira mwendo -kufikia kilele cha ufanisi

**Zozote 3X2**

(c) (i) baadhi walikubali kuhongwa/kuhonga –Asiya anapata kandarasi ya kuoka keki/Nguruma anapendelewa

(ii) Wanasagamoyo hawakuwa na umoja - baadhi waliwasaliti wenzao, Kombe na Boza wanajipendekeza kwa Kenga

(iii) Baadhi walishiriki katika matumizi ya vileo na kutokujua leo la kujikomboa

(iv) Baadhi ya Wanasagamoyo hawakuweza kutambua uongozi wa kike, walimchukia Tunu kwa vile alikuwa mwanamke-taasubi ya kiume

(v) Baadhi ya Wanasagamoyo hawakuwa na elimu iliyostahili, Ngurumo anamkumbusha Tunu kuwa walisoma pamoja na alipendelea Historia. Tunu alimpiku kimasomo

(vi) Kulikuwa na vitisho – Baadhi ya Wanasagamoyo waliandikiwa vijikaratasi vya kuwatishia kuhamishwa

(vii) Kulikuwa na mauaji ya wapinzani, Baadhi ya wanasagamoyo waliwaua wenzao ambao walipinga utawala dhalimu – Jabali

(viii) Utamaduni au desturi za kurithi mamlaka, Majoka alirithi uongozi kutoka kwa babake naye anataka kumrithisha mwanaye Ngao Junior/ Kenga anaudhika na hali hii.

(ix) Ukosefu wa ajira, walio na elimu bora wananyimwa nafasi za kuajira na uongozi wa Sagamoyo kwa vile ni tishio kwa nafasi zao. Wanakosa uwezo wa kifedha na kuishia kutegemea

(x) Wanasagamoyo kama Ngurumo wanashiriki kuwapiga wenzao na kuwaumiza, Tunu aliumizwa.

(xi) Vituo vya habari vya Wanasagamoyo vilivyowahamazisha vilifungwa na uongozi wa Sagamoyo – Runinga ya Mzalendo

(xii) Askari wa Sagamoyo walivunja mikutano ya Wanaharakati kwa amri ya Majoka

(xiii) Wanasagamoyo kama Kenga walimhimiza Majoka kuwatia mbaroni wapinzani wake, Ashua anatiwa ndani kwa kusudi la kumshurutisha Sudi.

**Zozote 10X1**

**2.** (a) (i) Maneno ya mwandishi/msimulizi UK114

(ii) anamrejelea Mwangeka

(iii) Ni katika ukumbi wa mikutano/warsha

(iv) Apondi alipomaliza hotuba yake, Mwangeka alikuwa hajiwezi tena kihisia alimpenda Apondi.

(b) (i) Mwenye bidii – masomoni

(ii) Amewajibika –

(iii) ana msimamo thabiti

(iv) Mzalendo

(v) Mvumilivu/mstahimlivu

(vi) mkarimu

(vii) Mnyenyekevu/mpole

(viii) mcheshi

(ix)

(c) (i) mapenzi/ ndoa/usuhuba – Mwangeka alianza kuhusiana na Apondi kimapenzi

(ii) ustahimilivu- Mwangeka hakutaka tena kuoa baada ya kifo cha mkewe

(iii) maombolezi/upweke- hali ya upweke na chuki kwa Mwangeka na Apondi kwa kufiwa na wapendwa wao

(iv) maridhiano/haja ya kuwa na amani- suala kusameheana na kuishi kwa amani

(v) wajibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali – Msalaba Mwekundu- kusaidia serikali katika kudumisha hali ya ushwari

(vi) Usawa wa kijinsia/ wanawake kupewa nafasi sawa/ Apondi anadhibiti wasilisho vilivyo - anashangiliwa

(vii) athari za vita – mke na watoto wa Mwangeka kuangamizwa/mme wa Apondi kufia vitani ughaibuni

(viii) utayarivu katika kupambana na mikasa/ raia au serikali wasitegemee

mashirika au wageni kuwaauni

(ix) walinda usalama kutagusana na raia kwa njia ya urafiki/salama/polisi wanastahili kushirikiana na raia bali si kuwadhalilisha

(x)

**Zozote 5X2**

**3.** (a) UK 64

**Umuhimu wa Annette**

(i) Anaonyesha watu waliokengeuka, wanathamini tamaduni za kigeni na kutukuzwa ugeni kuliko vya kwao
(ii) Athari anazopata mwanandoa mmoja anapoamua kugura ndoa – upweke/kifo
(iii) Udhaifu wa Kiriri kama bwana wa nyumba – anadhibitiwa na mkewe/anashindwa kumshawishi mkewe
(iv) Umuhimu wa kuwa na mashauriano katika ndoa ili iwafae wote kifamilia

(v) Imani kuwa ng'ambo kuna maisha mazuri – *Green Card* kuwa tikiti ya maisha mazuri

(vi) Mishahara iliyo midogo inawafanya wenyeji kuacha kazi na kwenda kuliko na mishahara mizuri.

(vii) Ukosefu wa uzalendo – Annette anaongozwa na ubinafsi-hajali nchi yake wala mmewe

(viii) Namna mzazi anavyoweza kuwaathiri watoto wake visivyo. Songoa anakashifu hali ya nchi yake/mawazo yake ni sawa nay a mamake

(ix) Elimu inayotolewa ni duni, elimu ya ughaibuni inathaminiwa na matajiri

(x) Anaonyesha umaskini uliopo nchini mwake ilhali hawa matajiri ndio wanaostahili kuimarisha nchi kiuchumi

Zozote 6X1

(b) (i) Ukabila- Selume/Subira wanabaguliwa na jamii zao kutokana na tofauti za kikabila. Kangata alikashifiwa na ndugu zake kwa kumwoza binti yake kwa watu wa ukoo 'mbaya'

(ii) mauaji- ndoa ya Ridhaa/Mwangeka/Apondi inaathirika kutokana na wenzao wa ndoa kuuawa

(iii) Uhalifu-ndoa ya Kaizari inatatizika kutokana na kutendewa unyama mkewe na mabinti zake mbele ya macho yake

(iv) Ndoa za lazima – Pete anaozwa kwa Fungo ambaye ni wa umri wa babu yake kwa lazima. Ndoa hii hatimaye inavunjika

(v) Ubakaji wa mabinti – Sauna anabakwa na baba mlezi. Mamake Sauna anamshauri asiliseme hadharani kwa vile ndoa yake itavunjika

(vi) Ndoa haramu – Nyangumi anaishi na Pete kwa majaribio akimwahidi kuwa atamwoa ilhali ana mke tayari. Anampachika mimba ambayo Pete anang'ang'ana kuitoa

(vii) Uasherati – Tenge anawaleta vimada kwa nyumba mbele ya wanawe pindi mkewe anapoenda shamba

(viii) Kuwakana wana – Babake Kipanga anamkana na kumfukuza kwake kuwa sura yake haifanani nay a wanawe wengine

(ix) Ukengeushi – Annette anamwacha mumewe Kiriri na kuhamia ughaibuni bila kujali hisia za mumewe/anamdhibiti mumewe.

(x)

**4.** i)

a) Kukonda -kwa kuugua na kulazwa
b) Njaa -kwa kushindwa kukaa
c) Vita -kwa kusababisha mvutano/ukosefu wa amani
d) Kifungo -kwa kutokuwa huru
e) Ukata/Umaskini -kwa kumkosesha pato la kujikimu
f) Ukiwa/Upweke -kwa kusababisha dhiki za ndani/kisaikolojia

(ii)

(a) Ningeulaani -ningeulaani
Ngawa -ingawa
Umuhimu- kupata urari wa mizani

(b) Kuuguwa -kuugua
Kuchaguwa-kuchagua
Umuhimu- kupata urari wa vina

(c) Kufinyanga sarufi

Hana haramu mkata- mkata hana haramu

Ukanikuta upweke-upweke ukanikuta

Umuhimu-kupata urari wa vina

Mfano-1

Umuhimu-1

3 ×2 =6

(iii ) (i) Mathnawi-vipande viwili kwa mishororo

(ii)Ukaraguni-vina vya kati na vya nje vinabadilika kwa kila ubeti

(iii)Sabilia-kila ubeti una kiishio/halina kibwagizo

3 ×1

(iv) Siwezi kusahau umaskini vilevile.Unasababisha mtu kukosa kipato cha kujikimu kimaisha.Maskani hana cha haramu daima huwa anaomba.

3 ×1

(v)

(i)Mishororo mitatu kwa ubeti

(ii)Vipande viwili kwa kila mshororo

(iii)Mizani 8×8 kwa kila mshororo

(iv)Vina vya ndani ni-ta na vya nje ni-ni

Za kwanza 3×1=3

**5.** (a) Mwanaume ambaye jamaa zake ni wahasiriwa wa ubakaji (alama 2x1)

(b) Kuonyesha namna watu mbalimbali wanavyoathiriwa na matendo ya ubakaji (alama 2x1)

(c) (i) Maswali balagha – na watoto kumewaka?

(ii) Nidaa – Kilichomtuma atake kujifungua! Siyahi

(iii) Taswira – Ya ubakaji

(iv) Kinaya – wabakaji kujitia kundini na kushangaa kilichomtuma atake kujifungua!

(v) Tasfida – wakachana mbuga na wake ubikira

(vi) Tabaini – si hapa walipomsurutisha mama. Si hapa sebuleni mwetu. Si hapa sokoni mwetu

(vii) Takriri – si hapa

(viii) Tashbihi – kama kuku wa kuchinja

(ix) Kuboronga sarufi – Shuleni alitoka na wangu mke mpendwa

(x) Chuku – mkoba wa kilo nzito za vitabu

(Zozote 5x1)

(d) (i) Taswira mnuso – maua ya kufurahisha pua

(ii) Taswira mguso – Walipiga miereka, kumburura shangazi, walimshika mkono

(iii) Taswira oni/mwono – binamu zangu wakiona

(iv) Taswira mwendo – wakachana mbuga na wake ubikira

(v) Taswira hisi – Baada ya yake sidiria kuikata?

– si hapa sebuleni mwetu?

(Zozote 4x1)

(e) (i) Toni ya uchungu – kwa jamaa ya nafsi heri kubakwa

(ii) Toni ya masikitiko – kubakwa kwa kichaa

(2x1)

(f) (i) Za yaliyojiri hapa

(ii) Na pua kufurahisha

(iii) Na kumfanya kufutia

(iv) Si hapa sokoni

(1x1)

(g) (i) Beti saba

(ii) Mishororo inatofautiana kwa kila ubeti

(iii) Vina vinatofautiana kwa kila ubeti

(iv) Mizani inatofautiana kwa kila mshororo

(v) Lina kipande kimoja kwa mshororo

(Zozote 4x1)

=alama 4

**6.** (a) (i) Maneno ya Jairo

(ii) Anamwambia Mwalimu Mosi
(iii) Nyumbani kwa Mwalimu Mosi
(iv) Mosi alimzawidi Jairo zawadi alizopewa; sasa Jairo naye ameona heri naye amletee zawadi mwalimu wake

(b) (i) Mwalimu Mosi aliwafunza wanafunzi wake kutobagua wenzao. Jairo alibaguliwa kwa kunyimwa fursa ya kutoa dukuduku lake

(ii) Jairo anamdhalilisha mwalimu wake kwa kumtolea cheche za maneno hadharani

(iii) Jairo hakuzingatia nasaha za Mwalimu Mosi. Aliishia kuwa miongoni mwa waliokosa kufaulu maishani

(iv) Jairo anawakashifu wenzake aliosoma nao. Anawaita majizi ilhali yeye mwenyewe hakutaka kufanya bidii shuleni

(v) Jairo anafurahia kustaafu kwa Mwalimu Mosi kwa vile anaona hakuna mtoto mwingine akayeathiriwa vibaya na Mosi huku Mosi anasifiwa kwa kuwakuza wanafunzi wengi

(vi) Jairo anamwona Mosi kama mwongo aliyewapa matumaini yasiyokuwepo

(vii) Jairo anaona kuwepo shuleni kulimpotezra wakati angekuwa mwizi hivyo kuishioa kuwa mtu wa maana zaidi katika jamii

(viii) Jairo alikatazwa pombe lakini yeye anaona kuwa ukisha lewa unaona raha ya maisha; eti hata ukiimia ukiwa mlevi huhisi uchungu.

(ix) ushauri wa kuwa muadilifu maishani, Jairo anaona usiyo na maana, anaona haramu kuwa tamu/ anaona maisha ni mafupi

(x) Jairo hakumshukuru Mwalimu kwa kumpelekea zawadi
(xi) Jairo aliwatukana waliotumwa kumpelekea zawadi
(xii) Jairo alichukulia kupelekewa zawadi kama jambo la kumdunisha/kumwaibisha ihali ni mhitaji
(xiii) Jairo anampa Mwalimu Mosi mke na watoto kama zawadi kutoka kwake

(xiv) Amamkosea heshima mke wake kwa kumtoa kama zawadi/bidhaa kwa mtu mwingine

(xv) Anamwingilia mwalimu kwa utundu mapema kwa kuipeleka aila yake kwa mwalimu pasipo kujali hisia za mwalimu na mke wake/alimdhalilisha mwalimu mbele ya mke wake

(xvi) Anafuata uvumi na kumvamia mwalimu kwa nia ya kumdhuru kwa upanga

(xvii) Hajui kuomba msamaha badala yake alipogundua makosa yake anataka kujitoa uhai

7(a)

**i.Kinaya**-Samueli anapuuzwa na mwalimu mkuu badala ya kupongezwa.

**ii.<u>Umuhimu wa Samueli</u>**

i. **Anabainisha uwajibikaji wa mwalimu mkuu** –anapothibitisha kuwa amemaliza karo ndipo anampa matokeo yake

ii. **Anabainisha maudhui ya taasubi za kiume /ubabedume** -babake kumwonea fahari mwanawe wa kiume akifua dafu.

iii. **Ni kielelezo cha ukosefu wa maadili -**kuchanganya mapenzi na masomo.

iv. **Ni kielelzo cha watu wanaokabiliana na changamoto za maisha kwa kujiua**- anapoanguka mtihani anajitosa majini ili afe.

v. **Anajenga maudhui ya elimu** –kufeli mtihani ni fedheha

vi. **Ni kielelezo cha watu wasiowajibika** –kuficha matokeo yake baada ya kufeli mtihani

(b) (i) kula kunawafanya Sasa na Mbura kuwa wategemezi; wakishiba hawafanyi lolote

(ii) Mzee Mambo ni waziri asiye na wizara maalum, analipwa mshara wa walipa kodi pasi kufanya kazi

(iii) Licha ya Mzee Mambo kutokuwa na wizara maalum yeye na wenziwe wanajiamulia kima cha mshahara watakaopokea

(iv) Mzee Mambo alipewa wadhifa huu kwa nia ya kuongeza walaji

(v) Dini inatumiwa kuhalalisha haramu/ulafi. 'Hadhaa min fadhil rabbi'

(vi) Wafanyakazi hufika kazini ila hawatendi kazi zenyewe lengo ni kuwepo

(vii) Wanabadhiri fedha za umma kwa sherehe chapwa; mtoto kuota meno/kuanza darasa la chekechea

(viii) wanajinadi kwa mitandao ili wajulikane ndio wafadhili wakuu na kupata sifa

(ix) Magari ya umma/ rasilmali inatumiwa yanatumiwa kwa shughuli za kibinafsi- kusomba maji/kuleta mapambo/kubeba jamaa

(x) Vyakula anuai vinaandaliwa ilhali raia wana njaa
(xi) Watu wanafika kula tu/ Sasa na Mbura wanakula duru kadhaa ilhali hawachangii chochote
(xii) Walaji hawajali asili ya chakula chenyewe/ wanafanyiwa hisani
(xiii) Wanaposhiba wanalala
(xiv) Kula kunawafanya kudharau vyakula vya kiasili kama mchele wa Mbeya; wanafisha kilimo chao kwa kuagiza basmati
(xv) Viongozi ni mafisadi, wanachota fedha za umma na hawajali kulaumiwa
(xvi) Dawa zinaibwa kutoka mabohari za serikali na kuuzwa katika maduka ya watu binafsi
(xvii) Kula huku kunasababisha maradhi kama sukari, presha, saratani
(xviii) Kula kunawafanya wauane kifikira na kimawazo/wananyang'ana vinavyoonekana na visivyoonekana

Zozote 12X1

**8)** a)

i) Ni kero hili si huba
ii) Mgani nataka kuishi nawe muluba oendo viraka viraka, linanishinda kuziba

b)

i) Mwenye tamaa – kupenda fedha/ pesa
ii) Mwenye ubinafsi – kujali pesa kuliko
iii) Msaliti – kupenda pesa badala ja fuata penzi
iv) Mwenye mapuuza – anapuuza penzi
v) Mgomvi – lala kulinena washako

Za mwanzo 3

c)

i) Jazanda/ sitiari – mimi pendo la mvika
ii) Takriri – Pendo viraka viraka, titani, shindo kuziba
iii) Inkisari – Wanasifika, walostarabika silaiye n.k
iv) Kuboronga sarufi – Nasomba vyangu viraka ingawa mno nataka
v) Mishata – Pendo viraka viraka

*Za kutuza nne*

d)

- Hutumiwa kuburudisha jamii.
- Hutumiwa kutakasa hisia za anayeamba kama vile huzuni.
- Hutumiwa kusifu/kukashifu tabia za mpenzi katika jamii.
- Hutumiwa kukuza ubunifu wa jamii ili kuibua hisia k.v huzuni, huruma n.k
- Ni nyenzo ya kupitisha maarifa au elimu ya jamii.

Zozote 5X1

e) i.

- Kufanya maandalizi – ili kujua walengwa, muda wa utafiti, gharama na mbinu za utafiti
- Kukusanya data kwa kupitia kwa hojaji, mahojiano, kushiriki ama kutazama.
- Kurekodi data kupitia kwa maandishi, kunasa sauti ya mhojiwa,
- Kuchunguza data upya/maelezo yaliyotolewa na kuyanakili jinsi yalivyo ili kuchanganua baadaye.
- Kuchanganua data na kufasi kwa matokeo ya uchunguzi kuhusu maigizo.

ZOZOTE 3X1

ii.

(i). Kupotea kwa sifa muhimu kama vile ishara, hisia, toni, kiimbo n.k
(ii). Kupotea kwa uhai asilia wa kutenda na kusema
(iii). Kukosa kwa ile taathira asilia kunanyima hadhira fursa ya kuuliza maswali na kushiriki
(iv). Kupunguza kwa hadhira na usambazaji wake.

Zozote 3x1